# Disciples' Network

Luka 10:19

**Jarida la kila Mwezi** **Toleo 011 - Julai, 2023**


## UTANGULIZI

Shalom mpendwa,
Tunamtukuza BWANA kwa kutujalia kuingia mwezi wa nane tukiwa washindi tena. Kwa neema yake ametuwezesha kutoa huduma za kiroho, kiakili na kimwili kwa watu wa dini zote, rika zote na makabila yote, ndani na nje ya Tanzania kwa mwezi Julai 2023, kupitia njia mbalimbali na pasipo kuchoka wala kuzimia mioyo. Hakika tumeweza kwa sababu Mungu yupo pamoja nasi naye ametutia nguvu na kutushika kwa mkono wake hodari. (Isaya 41:10).



## MAHUDHURIO

Idadi ya waliohudhuria ibada zetu mwezi Julai 2023 ni kama ifuatavyo:-

| | Arusha | DSM | Mwanza |
|---|---|---|---|
| Wanawake | 18 | 641 | 143 |
| Wanaume | 4 | 202 | 24 |
| Watoto | | 98 | 102 |
| Google Meet | | 4,146 | |

Jumla ya waliofikiwa na ibada zetu kwa mwezi Julai ni 5,404.


## WAONGOFU WAPYA


Kupitia ibada hizi watu 25 waliamua kumpa Yesu Maisha siku hiyo. Tunamtukuza Bwana na tunawaombea waweze kusimama kiroho na kuufurahia wokovu wa BWANA.

## MATUKIO


### (a) Ushuhuda


Tumekuwa na shuhuda nyingi za kusisimua ndani mwezi wa saba. Vijana wetu wengi wamefanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya NECTA ya kidato cha sita, wagonjwa wameponywa, watoto wachanga wamewekwa wakfu, watu wengi wamepata kazi, wengine wamepandishwa vyeo, ndoa zilizokuwa zivunjike zimepona, waliotamani kujiua wamerejeshewa hamu ya kuishi, wengi wamekutana na destiny helpers katika namna ya ajabu, wengi wamefunguliwa vifungo vizito vilivyowatesa muda mrefu, waliokuwa wamekoma siku zao za hedhi kabla ya wakati siku zimerejea, waliokuwa wamefungwa vipawa na karama wamefunguliwa, mitego ya kichawi mingi imeteguliwa, na shuhuda nyinginezo nyingi (zimetumwa katika makundi ya Whatsap ya huduma) Kimsingi kila mwenye bidii ya kufuatilia ratiba za ibada ameshuhudia matokeo ya kushangaza katika Maisha yake ya kiroho na kimwili.




Miongoni mwa shuhuda kubwa za ufungulivu zilizotolewa, ni ushuhuda wa kuponywa na kufunguliwa kwa mama mmoja aliyeteswa na uchungu kwa zaidi ya miaka 10 kutokana na maumivu ya mabaya aliyotendewa na mume wake kiasi cha kuona kama kifo ndio chaguo sahihi kwake. Alipata matatizo mbalimbali ya kiafya kwa sababu ya huo uchungu na hata ikafungua mlango wa adui kumshambulia binti yake. Kwa rehema na neema ya Mungu kupitia ubatizo uliofanyika tarehe 16/07/2023, mama huyu pamoja na binti yake walifunguliwa na kuponywa kiasi kwamba amani, upendo, furaha na baraka za Mungu zimefunguka kwenye familia yao. Sifa na utukufu tunamrudishia Mungu.



## (b) Ubatizo wa maji mengi




Tunamshukuru BWANA kwa neema yake kwa wana Disciples Network wa Dar es Salaam. Baada ya miezi kadhaa ya kusubiri, hatimaye tulipata kibali cha kuandaa ibada ya ubatizo iliyofanyika siku ya Jumapili tarehe 16/07/2023.

Ibada hii iliambatana na mafundisho ya ubatizo pamoja na ubatizo wa maji mengi ambapo watu 34 walibatizwa. Ishara na ajabu nyingi zilikuwa Dhahiri siku hiyo na shuhuda nyingi za mabadiliko kutoka kwa waliobatizwa zimeendelea kumiminika.

## (c) Singles in the wait session

Ashukuriwe Mungu kwa neema yake kwa vijana; ilifanyika semina ya mabinti na vijana wanaosubiri ndoa iliyokwenda kwa jina la THINGS I WISH I'D KNOWN BEFORE WE GOT MARRIED. Semina hii ilifanyika kwa njia ya Google Meet tarehe 23/07/2023 ambapo takribani vijana 85 walihudhuria mafunzo haya.

Ndani ya semina hii mada kuu mbili zilizojadiliwa ni; LIKE MOTHER LIKE DAUGHTER, LIKE FATHER LIKE SON na SOLVING DISAGREENMENTS WITHOUT ARGUING.

Mada hizi zililenga kuwaandaa vijana kuja kuwa kina mama na baba bora watakapoingia kwenye ndoa lakini pia vijana walifunzwa namna ya kutatua migongano bila mabishano.

## (d) Semina ya wanaotarajia kujiunga na elimu ya juu (vyuo na vyuo vikuu)

Tunamshukuru Mungu tarehe 27/07/2023 tulifanikiwa kuwa na semina elekezi kwa vijana wanaotarajia kujiunga vyuo vikuu ambapo vijana 40 waliweza kuhudhuria semina hiyo. Semina hii ilielekeza namna ya kuomba udahili katika vyuo, kuomba mkopo wa elimu ya juu, na udhamini wa elimu ya juu (Scholarship).



## (e) Darasa la afya

Kwa neema ya Mungu tulifanikiwa kuwa na darasa la Afya ya akili tarehe 17/07/2023 kwa njia ya Google Meet ambapo zaidi ya watu 100 walihudhuria na kuhudumiwa. Shukrani za pekee kwa Daktari na mkufunzi Deogratius Ramale aliyehudumu.

# HUDUMA YA MAOMBI

a) Maombi asubuhi ya kuamuru mapambazuko (Morning light)

Habari njema! Tunamshukuru Mungu tumefanikiwa kuanzisha maombi ya asubuhi ya kuamuru mapambazuo (The morning light). Maombi haya hufanyika kila Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 11:00 asubuhi hadi saa 11:30 asubuhi (Ayubu 38:12 ).

Huduma hii imepokelewa kwa shauku kubwa takribani watu 817 wameweza kuhudhuria ndani ya wiki mbili na imekuwa ni yenye manufaa na shuhuda kutoka kwa wanaoshiriki ibada hii ya kuamuru asubuhi.

b) Huduma ya maombi ya ana kwa ana na kwa njia ya simu

Tumefanikiwa kutoa huduma ya maombezi na ushauri ana kwa ana na kwa njia ya simu kwa watu waliopo Dar es salaam na mikoa mbalimbali.

Hii ni pamoja na kupokea simu za wanafunzi walioko ndani ya Dar-es-Salaam na mikoani wenye uhitaji wa kihuduma kama vile ushauri, maombi na maarifa ya neno la Mungu.

# MAMBO YAJAYO

Maandiko yanatuambia tuombe bila kukoma, 1Thes. 5:16-18, tunaomba maombi yako kwa ajili ya yafuatayo:

- Ombea utekelezaji wa mipango na mikakati ya kumzalia Bwana Yesu matunda zaidi. Vile vile ombea uchumi wa huduma na ikikupendeza tafadhali tusapoti kifedha ili tuendeshe shughuli za huduma kwa wepesi.
- Mfungo wa siku tatu kwa watenda kazi Maandalizi ya mfungo wa Daniel
- Ombea wagonjwa wote na wenye shida mbalimbali.
- Ombea sherehe ya watoto itayofanyika mwezi huu wa nane tarehe 11 mwezi Agosti, 2023. Ombea semina ya vijana wadogo(teenagers),-Jumamosi ya mwisho wa mwezi Agosti 2023.



# RATIBA ZA IBADA



Tunakualika kushirikiana katika kueneza Injili ya YESU Kristo. Vile vile tunakualika wewe na familia yako, ndugu, jamaa na marafiki kujiunga nasi kwenye ibada zetu ambazo hufanyika Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

| MAHALI | SIKU | TUKIO | MUDA |
|---|---|---|---|
| Dar-es-Salaam | Jumatano | Maombi | 11:30 Jioni |
| | Ijumaa | Mkesha Online | 05:00 Usiku |
| | Jumamosi | Fellowship | 07:00 Mchana |
| Mwanza | Jumanne Jumatano na Alhamisi | Maombi kwa kupitia Google Meet | 04:00 Usiku |
| | Jumamosi | Fellowship | 07:00 Mchana |
| Arusha | Jumanne | Fellowship | 11:00 Jioni |
| | Jumamosi ya mwisho wa Mwezi | Fellowship | 07:00 Mchana |

# MAWASILIANO

Dar es salaam
+255 755 999 198 / +255 687 222 197

Mwanza
+255 753 853 493

Arusha
+255 717 108 306

DISCIPLES' NETWORK

DNETWORK

DISCIPLESNETWORK

DISCIPLES' NETWORK